Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
**Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia**

# ELIMU Bulletin

JARIDA LA MTANDAONI: Toleo Na.37 - 2024

wizara_elimuTanzania wizara_elimuTz www.facebook/moestvt.com www.wyestu.blogspot.com www.moe.go.tz ELIMUTZ

*Tunaboresha Elimu Yetu*




## Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 Toleo la 2023 Sasa Rasmi



# Samia akoshwa na ubora wa Jengo Mtambuka la Mafunzo SUA

## - KAZI IENDELEE -




## BODI YA UHARIRI

Sylvia Lupembe
***Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini***

**Wachangiaji:**
Oliva Kato
Elizabeth Pancras
Veronica Chitunda
Nazareth Mwakabuta

**Mawasiliano:**
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
Mji wa Serikali Mtumba, Mtaa wa Afya - Dodoma
S.L.P. 10, 40479 DODOMA.
Simu: +255 26 296 3533

**Jarida hili linatolewa na**
Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

# TAHARIRI

## WATAALAM WA SAYANSI NA TEKNOLOJIA NI NGUZO YA UCHUMI

Maendeleo ya Sayansi na Teknolojia yameleta athari chanya katika sekta mbalimbali Nchini Tanzania, kama ilivyo katika mataifa mengine Duniani. Mathalan katika sekta ya elimu ambapo yamechangia kuwezesha ufundishaji na ujifunzaji kwa makundi yote katika ngazi mbalimbali za elimu.

Kadhalika maendeleo hayo yamechagiza ongezeko la fursa za ajira katika sekta mbalimbali za kijamii na kiuchumi ikiwemo Elimu, Afya, Kilimo, Nishati Usafirishaji na Mawasiliano.

Kwenda sambamba na mabadiliko hayo, Serikali ya Tanzania kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeendelea kuimarisha fursa za upatikanaji wa elimu katika ngazi zote. Fursa zilizoimarishwa ni pamoja na kutoa mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu kupitia Samia Skolashipu inayowalenga Wanafunzi wanaosoma fani za Sayansi, Teknolojia, Uhandisi, Hisabati na Sayansi za Tiba.

Akizungumza katika Maadhimisho ya Miaka 50 ya Idara ya Ujenzi ya Chuo cha Sayansi na Teknolojia Karume (KIST) Agosti 27, 2024 Visiwani Zanzibar Waziri Mkuu Mhe. Kassim aliwahimiza Watanzania kuchangamkia fursa za mafunzo katika fani za Sayansi na Teknolojia ambazo zinapewa kipaumbele na Serikali ili kuchochea maendeleo.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amesema katika kuhamasisha Wanafunzi kusoma fani za Sayansi, Samia Skolashipu inatoa mikopo ya asilimia miamoja kwa wanaofaulu vizuri masomo ya Sayansi kidato cha Sita na kwamba Rais Mhe. Samia Suluhu Hassan ameongeza fedha za Mikopo kutoka bilioni 464 hadi Bilioni 787, ameongeza kuwa fedha hizo zitaendelea kuongezeka.

Pia ikumbukwe Mwaka wa fedha 2024/25 Serikali imetenga jumla ya Shilingi bilioni 1.6 kupitia Samia Extended Skolaship, kuiwezesha Tume ya Nguvu za Atomu Tanzania (TAEC) kufadhili Wanafunzi kwenda Nje ya Nchi kusoma Shahada ya Uzamili katika fani zinazohusiana na teknolojia ya Nyuklia, ikilenga kuongeza idadi ya wataalamu wa nyuklia na mionzi.



Miundombinu Bora >



# Rais Samia akoshwa na ubora wa jengo mtambuka la mafunzo SUA

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan amesema Serikali itaendelea kuunga mkono Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) katika utekelezaji wa majukumu yake, kwa kuzingatia dhamira inayolenga kuongeza tija ya uzalishaji mashambani.

Rais Samia ametoa kauli hiyo Agosti 06, 2024 baada ya kuzindua jengo Mtambuka la Mafunzo la Chuo hicho, ambalo limejengwa kwa fedha zilizotolewa na Serikali pamoja na mapato ya Chuo hicho na kwamba amefurahishwa na ubora wa jengo hilo.

"Naipongeza Wizara na Uongozi wa Chuo, Serikali imetoa fedha kama bilioni 9 hivi, lakini mkajiongeza mkaongeza zaidi ya bilioni **2**, hii ni hatua kubwa sana kuelekea Chuo kujitegemea, hongereni SUA kwa kazi nzuri mliyofanya" alisema Rais Samia.

Aidha Rais Samia amekipongeza Chuo hicho kwa kuendelea kuzalisha Wataalam wanaotoa huduma za kijamii katika maeneo mbalimbali, akisema wanapata masomo ya viwango vya juu na kwamba amefurahishwa kuona wageni kutoka Mataifa mbalimbali wakijifunza hapa nchini.

"Hii ni fahari yetu kama nchi, huko nyuma tulikuwa tunatoka sisi kwenda kwa wenzetu kujifunza, lakini leo siyo kwa SUA peke yake, hata vyuo vingine ambapo wageni wanakuja kwetu kusoma, hii ni hatua kubwa kwa Taifa" alisema Mhe. Samia.

Jengo Mtambuka la Mafunzo SUA limejengwa kwa gharama ya zaidi ya Sh. bilioni **11.7**, ambapo fedha kutoka Serikali Kuu ni zaidi ya Sh. bilioni **9.038** na zaidi ya Sh. bilioni **2.668** zimetokana na mapato ya ndani ya chuo.

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan Agosti 6, 2024 amezindua jengo Mtambuka la Mafunzo la Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA)

Jengo hilo lina madarasa nane, Ofisi kumi na moja, Maabara nane na Vyumba vya Kuhifadhia Kemikali saba pia jengo hilo lina uwezo wa kuchukua wanafunzi **3,205** kwa mara moja.



Samia Skolashipu>

# Pelekeni salamu fursa ya Samia Skolashipu - Mkenda

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amesema Serikali inatoa mkopo kwa asilimia miamoja kwa Wanafunzi wanaofaulu zaidi masomo ya Sayansi kidato cha Sita na kusomea nyanja za Sayansi, Elimu Tiba, Uhandisi, Hisabati na TEHAMA vyuo vikuu.

Waziri Mkenda amesema hayo Agosti 24, 2024 baada ya kuzindua Skuli ya Sekondari ya Kizimkazi Dimbani na Dahalia ya Wanafunzi wa kike katika Skuli hiyo Kisiwani Unguja, akiwasisitiza Walimu kuwahimiza Wanafunzi kutumia fursa hiyo kikamilifu.

Aidha ameipongeza Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kwenda sambamba na kasi ya uendelezaji wa elimu ambayo ndio mwelekeo wa Serikali inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

"Katika mageuzi haya ya elimu tuliyoanzisha, tuna mambo mengi ya kujifunza kutoka Zanzibar ya jinsi mnavyotekeleza. Tunahimiza elimu ujuzi na hapa tumetumia istilahi ya Amali ambayo hapa Zanzibar ndio inatumika" alibainisha Prof. Mkenda.

Awali akizungumza katika hafla hiyo, Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar Bw. Khamis Abdulla Said amesema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imegharamia kwa asilimia miamoja mradi wa ujenzi wa Skuli ya Sekondari Kizimkazi Dimbani kwa kutumia fedha za direct indicators, ambapo jumla ya Sh. Milioni 223 zimetumika.

Bw. Abdulla amesema mradi huo unajumuisha madarasa manne, chumba cha maabara na maktaba, ofisi ya Mwalimu Mkuu na Ofisi ya Walimu na kwamba itakuwa na uwezo wa kutoa Wanafunzi 180 kwa wastani wa Wanafunzi 45 kila darasa.





Rasimali Watu yenye Ujuzi >




# Mageuzi ya Elimu yanalenga kuwa na Rasilimali Watu yenye ujuzi



Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Phillip Mpango amesema Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kufanya mageuzi makubwa katika sekta ya elimu, yanayolenga kuongeza ubora wa elimu pamoja na kuandaa rasilimali watu yenye ujuzi itakayoendana na mahitaji ya Dunia ya sasa.

Akifungua Mkutano wa Elimu wa Kikanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Sherehe za Mwaka wa Elimu wa Umoja wa Afrika 2024, uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Arusha (AICC) Agosti 13, 2024 Mhe. Mpango amesema kuwa Mataifa ya Afrika Mashariki yanapaswa kuongeza uwekezaji katika sekta ya elimu ili kukidhi mahitaji ya utoaji elimu bora kwa watu wake.

Aidha Mhe. Mpango ameongeza kuwa mwenendo wa ongezeko la idadi ya watu katika Mataifa ya ukanda huo, unatoa ishara ya ulazima wa kuongeza rasilimali zaidi za kifedha ili kuhakikisha inaandaa vijana mahiri watakaoshiriki katika sekta mbalimbali za uzalishaji kukuza uchumi.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amesema mkutano huo ni fursa nzuri kwa nchi za Afrika Mashariki kubalishana uzoefu na kujifunza kutoka kwa mataifa mengine namna nzuri ya kuendeleza sekta ya Elimu.

Prof. Mkenda ameeleza kuwa Tanzania imeanza utekelezaji wa mageuzi katika ngazi zote za elimu na kwamba lengo kuu ni kuhakikisha Taifa lina jenga nguvu kazi yenye ujuzi na umahiri.

Mkutano huo ulihudhuriwa na Viongozi mbalimbali wa Umoja wa Afrika, Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mawaziri wa Elimu na Wawakilishi kutoka nchi Wanachama Afrika Mashariki, Wadau wa Maendeleo, Mashirika ya Kimataifa pamoja na Wadau wa Sekta ya Elimu.

Fursa za Elimu Juu >

# Majaliwa ahimiza kuchangamkia fursa fani za Sayansi na Teknolojia

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa amewataka Vijana wa Kitanzania kuchangamkia fani za Sayansi na Teknolojia ambazo zinapewa kipaumbele na Serikali ili kuzalisha wataalam wa kutosha watakaoshiriki katika sekta mbalimbali za uzalishaji.

Mhe. Majaliwa ametoa rai hiyo Agosti 27, 2024 akizungumza katika sherehe za Miaka 50 ya Idara ya Ujenzi ya Chuo cha Sayansi na Teknolojia Karume (KIST) visiwani Zanzibar, ambapo amesema katika kuongeza fursa za mafunzo kwa Wanasayansi Serikali inatekeleza mpango wa internship kuwawezesha wanafunzi kwenda kwenye makampuni mbalimbali kupata ujuzi kazini.

"Serikali inaendelea kuweka msisitizo suala la elimu ambapo katika Mwaka wa fedha 2024/25 imetenga Sh. bilioni 787 kwa ajili ya mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu" alisema Mhe. Majaliwa.

Waziri Mkuu ameipongeza Taasisi ya KIST kwa kuzalisha wataalam wanaoshiriki katika sekta za viwanda na ujenzi.

Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amesema Wizara inaendelea kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, ikiwemo Samia Skolashipu inayotoa ufadhili wa asilimia miamoja kwa Wanafunzi wanaosomea fani za sayansi.

Sambamba na hayo Waziri Mkenda amesema kuwa Wizara inatekeleza mradi ujulikanao Tanzania Education Labour Market Support unaolenga kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia pamoja na kuboresha programu za mafunzo ya ufundi katika uhifadhi wa mazingira na nishati endelevu.

Mradi huo unatekelezwa katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Karume (KIST), Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT), Chuo cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) na Chuo cha Ufundi Arusha (ATC).



Mafanikio Sekta ya Elimu >



# Rais Mwinyi akoshwa na mafanikio katika sekta ya elimu

Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar Mhe. Dkt. Hussein Mwinyi amesema Serikali itaendelea kuwekeza katika kuboresha miundombinu ya Elimu kuwezesha mazingira rafiki ya ujifunzaji, kuongeza fursa za mikopo na kuzingatia maslahi bora kwa Walimu.

Rais Mwinyi amesema hayo Agosti 26, 2024 Ikulu Zanzibar, akizungumza katika halfa ya kuwapongeza Wanafunzi waliofaulu kwa kupata daraja la Kwanza katika Mtihani wa Kidato cha Nne 2023 na Kidato cha Sita 2024 upande wa Unguja, ambapo ameeleza kuwa amefarijika kuona matokeo chanya ya uwekezaji katika sekta ya elimu.

"Natambua kuwa matokeo ya uwekezaji katika sekta ya elimu huwa hayaonekani haraka, lakini Wizara hii imefanya kazi nzuri na tumeanza kuona matokeo ya uwekezaji wetu mapema, hivyo nawapongeza sana" Alisema Rais Mwinyi.

Aidha Dkt. Mwinyi ameishukuru Serikali kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikiana kwa karibu sana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar katika masuala mbalimbali ya utekelezaji wa mageuzi ya Elimu.

Akizungumza katika hafla hiyo Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amewasisitiza Wanafunzi hao kutumia fursa ya mikopo ya elimu ya Juu, ikiwemo Samia Skolashipu ambayo imekuwa kivutio kuhamasisha Wanafunzi wenye uwezo mkubwa katika Sayansi kuendelea kusomea fani hizo ambazo zinalenga kuchochea ustawi na maendeleo ya Taifa.

"Katika kutekeleza ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na maelekezo ya Rais, Samia Skolashipu inatoa ufadhili asilimia mia moja kwa Wanafunzi waliofaulu zaidi kidato cha Sita na watakaosomea nyanja za Uhandisi, Elimu Tiba, Sayansi, Hisabati na TEHAMA na niwahakikishie mikopo na Ufadhili wa Samia unatolewa kwa kufuata vigezo vilivyowekwa" amesema Waziri Mkenda.

Aidha amebainisha kuwa, Mhe. Samia Suluhu Hassan ameongeza fedha za Mikopo kutoka Bilioni 464 hadi Bilioni 787 na kwamba zitaendelea kuongezeka ili kuwezesha wanafunzi wengi wenye vigezo kupata mikopo.

Pongezi Bodi >



# Prof. Nombo aipa kongole Bodi ya ADEM

Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Carolyne Nombo amei-pongeza Bodi ya Ushauri ya Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM) iliyomaliza muda wake kwa kufanya kazi nzuri ya kuishauri Wizara juu ya usimamizi na uendeshaji wa Wakala huo kwa kuzingatia malen-go yake.

Prof. Nombo amesema hayo wakati wa uzinduzi wa Bodi mpya ya Ushau-ri ya ADEM, ambapo ameeleza kuwa kupitia ushauri wa Bodi, Serikali imewe-za kupitisha mipango mbalimbali ya Wakala inayohusu usimamizi wa fedha, rasilimali watu pamoja na ushauri juu ya uongozi wa shule na taasisi za elimu.

"Usimamizi mzuri wa Bodi ume-saidia Wakala kufanikiwa kupata Hati safi kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) nawapongeza sana". Alisema Prof. Nombo.

Aidha Prof. Nombo amesema Bodi mpya inayoingia ina jukumu la kufua-ta nyayo ya Bodi iliyopita na kuongeza kasi zaidi katika kusimamia uendesha-ji wa Wakala kutekeleza majukumu yake, ikiwa ni pamoja na kushauri juu ya maslahi ya wafanyakazi, tathimini ya utendaji kulingana na malengo na vipa-umbele.

Ameongeza kuwa kuzinduliwa kwa Bodi hiyo kunakamilisha uundwaji wa uongozi wa ADEM baada ya kukamilika kwa mchakato wa uteuzi wa Mtendaji Mkuu ambaye ni Dkt. Maulid Jumanne Maulid.

Bodi mpya inaundwa na Dkt. Leon-ard Douglas Akwilapo - Mwenyekiti, Katibu Mkuu Mstaafu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Bw. Mwanyika Semroki - Kaimu Mkaguzi Mkuu wa Ndani kutoka Wizara ya Fedha, Bi. Jane Simon Kaji -Mkurugenzi Msaidizi Seh-emu ya Miundo ya Wakala za Serikali - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dkt. Co-letha Luoga Komba - Mhadhiri Mwand-amizi kutoka Chuo Kikuu Mzumbe.

## Mjadala Rasimu ya Elimu >

# Wadau wajadili Rasimu ya Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Elimu



Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imekutana na wadau ili kupokea maoni ya Rasimu ya Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Elimu 2021/22 - 2025/26 yatakayowezesha kufikia malengo, shabaha na kutekeleza mikakati ya kuendeleza Sekta ya Elimu nchini.

Akizungumza Agosti 19, 2024 Jijini Dar es Salaam katika ufunguzi wa mkutano wa wadau hao, Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Dkt. Wilson Charles amesema kuwa rasimu ya mpango huo imeandaliwa na kikosi kazi maalum, hivyo mkutano huo unalenga kupata maoni kutoka kwa wadau ili kuiboresha rasimu hiyo.

Dkt. Charles amesema kuwa ni muhimu kwa wadau hao kutoa maoni kwa kuzingatia mabadiliko katika sekta ya elimu ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya Sera ya Elimu na Mafunzo, Mitalaa na pia kuzingatia taarifa ya sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022.

Akizungumza katika Mkutano huo Mwenyekiti wa kundi la wadau wa Maendeleo na Mkuu wa Kitengo cha Elimu Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) Bi. Faith Shayo ameipongeza Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kushirikisha wadau kutoka maeneo mbalimbali ikiwemo wanafunzi wa Msingi na Sekondari, Vyuo vya Elimu ya Juu na Kati katika mkutano huo.

"Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu ni wetu sote na nina furaha kuona pia umekuwa shirikishi hivyo unawapa wadau mbalimbali nafasi kuuangalia, kuuelewa na kutoa maoni ili utuongoze kwa miaka mitano tukiwa na uelewa na nia moja," amesisitiza Shayo.



Kubadilisha Mifumo ya Elimu >




# Prof. Mkenda: Mifumo ya Elimu lazima ibadilike ili kufikia malengo



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Adolf Mkenda amesema katika ulimwengu unaobadilika kwa kasi, mifumo ya Elimu Nchini lazima ibadilike ili kufikia malengo kwa kuwapatia vijana ujuzi, maarifa na maadili kuwawezesha kustawi na kuhimili ushindani katika karne ya 21.

Mkenda amesema hayo Agosti 15, 2024 wakati akifungua Mkutano wa Elimu wa Kikanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Sherehe za Mwaka wa Elimu wa Umoja wa Afrika 2024 uliofanyika katika ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Arusha (AICC).

Amesisitiza kuwa ni lazima tuhakikishe kuwa Elimu inayotolewa haihusu mafanikio ya Kitaaluma pekee, bali kuhakikisha inawezesha kwenda sambamba na mabadiliko ya Teknolojia pamoja na mabadiliko ya tabianchi.

"Tunasisitiza umuhimu wa teknolojia, mageuzi ya sera na ushirikiano ili kubadilisha mifumo ya elimu yenye kuwaandaa vyema vijana kwa ajili ya siku zijazo" Alisema Prof. Mkenda.

Waziri Mkenda amesisitiza kuwa Tanzania inaendelea na utekelezaji wa mageuzi katika sekta ya elimu ili kuandaa vijana mahiri watakaoenda na mabadiliko ya kiteknolojia, uhitaji wa soko la Kitaifa na Kimataifa na pia kuzingatia suala la mabadiliko ya tabianchi.

Takwimu za Elimu Afrika >

# Nombo ateta na wadau kuhusu Mradi wa Takwimu za Elimu Afrika





Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Prof. Carolyne Nombo Agosti 12, 2024 Jijini Dodoma amekutana na wadau wa elimu kutoka Chama cha Maendeleo ya Elimu barani Afrika (ADEA) waliofika kutambulisha mradi wa ukusanyaji Takwimu za Elimu na Ustadi Afrika.

Ujumbe huo umemweleza Katibu Mkuu kuwa mradi huo utafanya kazi katika nchi 30 za Afrika kwa kipindi cha miaka mitano ukiwa na lengo la kuandaa na kukusanya taarifa zenye ubora ili kufanikisha ufuatiliaji wa maendeleo ya elimu.

Prof. Carolyne Nombo ameridhishwa na Mradi huo kwa kuwa Tanzania imeanza utekelezaji wa mitaala na Sera mpya ya elimu na kwamba Mradi huo utasaidia na kuwa chachu ya kukusanya Taarifa za wanafunzi kuanzia ngazi ya Elimu ya Awali hadi Elimu ya Juu mpaka katika soko la ajira.

Prof. Nombo amewaeleza kuwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia sasa imeanza kutekeleza mfumo wa kuwa na taarifa muhimu za elimu Nchini (Basic Statistics in Education) ambazo zitakuwa zinatolewa kila mwaka na Wizara ikiwa na takwimu na taarifa muhimu za kielimu za ngazi zote za elimu.

Katibu Mkuu amewataka wajumbe hao kutembelea Taasisi mbalimbali zinazojihusisha na masuala ya ukusanyaji wa taarifa ikiwemo Taasisi kama Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA), Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Eastern Africa Statistical Training Center (EASTC) na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

# Anuani za Taasisi zilizo chini ya Wizara

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU),**
Jengo la Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia,
S.L.P 6562,
7 Mtaa wa Magogoni,
11479 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2113694, 2113691
Barua Pepe: es@tcu.go.tz

---

Mkurugenzi Mtendaji,
**Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB),**
HESLB House, 1 Mtaa wa Kilimo -TAZARA,
Barabara ya Mandela,
P.O. Box 76068,
15471 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 736 665 533/ 739 665 533
Baruapepe: ed@heslb.go.tz

---

Katibu mtendaji,
**Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA),**
Eneo la Viwanda Mikocheni,
Barabara ya Bagamoyo,
S.L.P 2624 au 32019,
14112 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2700493-6/9 na 22 2772423
Barua Pepe: esnecta@necta.go.tz

---

Mtendaji Mkuu,
**Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTVET),**
S.L.P 17007, DODOMA.
Simu: +255 26 2323 121 / 0733 77 77 51
Barua Pepe: info@nacte.go.tz

---

Mtendaji Mkuu,
**Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM),**
Nunge Street, Old Catholic Church Road,
S.L.P 71, BAGAMOYO, PWANI.
Simu: +255 23 244 0216
Barua Pepe: adem@adem.ac.tz

---

Mkurugenzi Mkuu,
**Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH),**
Barabara ya Ali Hassan Mwinyi,
S.L.P. 4302,
14113 Kijitonyama,
DAR ES SALAAM.
Simu: +255 (022) 2771358/ 2774023/ 2700749
Baruapepe: dg@costech.or.tz

---

Mkurugenzi Mkuu,
**Taasisi ya Elimu Tanzania (TET),**
Plot 132, Barabara ya Ali Hassan Mwinyi
S.L.P. 35094, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 0735 041168
Barua Pepe: director.general@tie.go.tz

---

Mkurugenzi Mkuu,
**Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA),**
S.L.P 34578,
Mikocheni B, Bima Road,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Barua Pepe: info@tea.or.tz
dg@tea.or.tz

---

Mkurugenzi Mkuu
**VETA Makao Makuu,**
Plot No. 18, Central Business Park (CBP)
Barabara ya VETA,
S.L.P 802,
26 DODOMA.
Simu: +255 26 2963661
Baruapepe: info@veta.go.tz

---

Mtendaji Mkuu,
**Tume ya nguvu za Atomic Tanzania (TAEC)**
S.L.P 743,
23114 Engutoto, Block J, Plot No 216,
ARUSHA
Simu: +255 272 9700054
Barua Pepe:dg@taec.go.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM),**
Kampasi ya Mwalimu Julius Nyerere Mlimani,
S.L.P. 35091, Mtaa wa Chuo Kikuu
16103 Dar es Salaam
Simu: +255222410700
Baruapepe: vc@udsm.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Ardhi University (ARU),**
Plot No. 3, Observation Hill Blok L,
University Road,
P.O. Box 35176, DAR ES SALAAM.
Simu: +255 738 357 310-12
Baruapepe: aru@aru.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi, Muhimbili (MUHAS),**
9 Barabara ya Umoja wa Mataifa,
Upanga Magharibi,
S.L.P. 65001,
11103 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2150302-6
Baruapepe: vc@muhas.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA),**
S.L.P 3000,
Barabara ya Edward Moringe, Mtaa wa Kilimo,
01 MOROGORO
Simu: +255 23 260511-4
Barua Pepe: sua@sua.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Mzumbe (MU),**
S.L.P 1, MOROGORO
Simu:
Barua Pepe: mu@mzumbe.ac.tz
info@mzumbe.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM),**
S.L.P 259,
Mtaa wa Benjamin Mkapa,
Jengo la Benjamin Mkapa,
41107 DODOMA.
Simu: +255 26 2310001/2/3
Barua Pepe: vc@udom.ac.tz
relations@udom.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Huria Tanzania (OUT),**
S.L.P. 23409,
14110 Open University Road,
Kinondoni Municipality,
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2668820/ 2668992
Baruapepe: vc@out.ac.tz

---

RASI wa Chuo,
**Chuo Kikuu kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE),**
Taifa Road Next to Benjamin Willium,
S.L.P 2329,
15105 DAR ES SALAAM.
Simu: +255 22 2850975
Barua Pepe: principal@duce.ac.tz
dpacademic@duce.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ushirika Moshi,**
06 Barabara ya Sokoine Moshi,
S.L.P 474
KILIMANJARO
Simu: +255 272 751 833
Barua Pepe: info@mocu.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kushiriki Cha Elimu Mkwawa (MUCE),**
Mtaa wa Mkwawa Chuo,
S.L.P. 2513,
51111 IRINGA CBD.
Simu: +255 26 2702 751
Baruapepe: principal@muce.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu Cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST),**
S.L.P. 131,
Barabara ya 01 MUST,
01 MBEYA.
Simu: +255(0)25 2957542/4
Barua pepe: vc@mustnet.

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (NMIST),**
Kampasi ya Tengeru, Barabara ya Nelson Mandela,
S.L.P. 447,
23301 TENGERU, ARUSHA
Simu +255 272970001
Baruapepe: vc@nm-aist.ac.tz

---

Makamu Mkuu wa Chuo,
**Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius Kambarage Nyerere,**
S.L.P 976, Butiama, MARA
Simu:
Barua Pepe: info@mjnuat.ac.tz

---

Mkurugenzi
**Bodi ya Huduma za Maktaba (TLSB),**
27 Mtaa wa Bibi Titi Mohamed,
S.L.P 9283
DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2150048/9
Barua Pepe: info@tlsb.go.tz

---

Katibu Mtendaji,
**Tume ya Taifa ya UNESCO,**
7 Magogoni Street,
P. O. Box 20384,
11479 DAR ES SALAAM
Simu: +255 22 2126598/ 22 2134292
Baruapepe: info@natcom.go.tz

---

Mkurugenzi,
**Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)**
23 Mtaa wa Bibi Titi Mohammed,
S.L.P. 20679,
11103 DAR ES SALAAM
Simu:
Baruapepe: info@iae.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Ufundi Arusha (ATC),**
Junction of Moshi-Arusha and Nairobi Roads,
P.O. Box 296,
23105 ARUSHA.
Simu: +255 (0) 27-297 0056
Baruapepe: rector@atc.ac.tz/pro@atc.ac.tz

---

Mkurugenzi,
**Kituo cha Maendeleo Dakawa,**
S.L.P 1733,
MOROGORO.

---

Mkuu wa Chuo,
**Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT),**
Kona ya Bibi Titi na Barabara ya Morogoro
S.L.P 2958
11104 DAR ES SALAAM
Simu:
Barua Pepe: principal@dit.ac.tz

---

Mkuu wa Chuo,
**Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA),**
30 Barabara ya Kibada,
S.L.P 9193,
17107 Kigamboni,
DAR ES SALAAM.
Simu:
Baruapepe: rector@mnma.ac.tz